

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



Kumb.Na. DC. 11/71/03/119

25 Oktoba, 2021

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera anakaribisha Maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi 31 kama zilivyobainishwa katika Tangazo Hili.

1. MTAKWIMU NAFASI 31

Eneo la Kazi: Biharamulo (3), Bukoba DC (6), Bukoba Mc (2), Karagwe Dc (3), Kyerwa Dc (5), Missenyi DC (2), Muleba DC (7) na Ngara DC (3)

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe amehitimu elimu ya Kidato cha Nne (IV) au cha Sita (VI)
- ii. Awe Mtanzania, mwenye Umri kuanzia Miaka 18 au Zaidi na asiwe na Umri unaozidi miaka 45
- iii. Awe na Stashahada /Stashahada ya juu/ Shahada ya Tehama (IT), Utunzaji wa Kumbukumbu au fani yoyote inayoendana
- iv. Awe na uzoefu usiopungua Mwaka mmoja kazini wa uingizaji wa Takwimu kwenye Mfumo.
- v. Awe na uwezo na ujuzi wa mawasiliano
- vi. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea na kwa kushirikiana wa watumishi wengine
- vii. Awe na uwezo wa Kutunza siri za Ofisi
- viii. Awe na uwezo na Ujuzi wa uchambuzi wa Takwimu, utatuzi wa matatizo na Ujuzi wa Taasisi (organisational skills)

1.2 KAZI NA MAJUKUMU

- 1) Kuingiza takwimu/taarifa za kitabibu,maabara na fomu mbalimbali kwenye mfumo wa Takwimu chini ya usimamizi wa Mratibu wa takwimu wa wilaya na kuripoti kwa Kiongozi wa CTC
- 2) Kuandaa,Kupitia na kushirikisha taarifa mbalimbali za Kila wiki,mwezi na robo mwaka
- 3) Kuandaa na kufanya uchambuzi wa wateja wanaohitajika kufuatiliwa baada kukosa miadi mfano LTFU, Viral load
- 4) Kufanya uchambuzi na kutafsiri takwimu katika kituo ili ziweze kutumika katika upangaji wa mipango na maamuzi mbalimbali.
- 5) Kutoa taarifa za fomu zenyе changamoto
- 6) Kuhudhuria Vikao mbalimbali watakapohitajika
- 7) Kutoa mawasilisho ya mapendekezo ya uboreshaji wa uingizaji wa Takwimu katika Mfumo.
- 8) Kufanya kazi zingine za takwimu atakazopangiwa na Msimamizi wa Kazi.
- 9) Kutoa taarifa za changamoto za Mfumo wa takwmimi kwa msimamizi wa takwimu ndani ya dakika 15 baada ya Ugunduzi wa Changamoto
- 10) Kufanya usuluhishi wa kitakwimu na Kuangalia usahihi wa takwimu kwa kutu,ia vyanzo vya taarifa
- 11) Kuendana na Viwango vya maadili na Kuwajulisha Viongozi wa CTC juu ya Ukiukwaji wa maadili
- 12) Kuendana na sera za kiutawala na rasimali watu

1.3 UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

- a) Maombi yote yatumwe kwa anuanii hii
**Katibu Tawala Mkoa,
S.L.P 299,
BUKOBA.-KAGERA**
- b) Maombi yaambatanishwe na vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA
- c) Kila mwombaji aambatanishe wasifu wake CV

1.4 MWISHO WA KUTUMA MAOMBI

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 8/11/2021


PRM. Rubanzibwa
KAIMU KATIBU TAWALA(M)
KAGERA